ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

*Supplement No. 6* *17th October, 2023*

## *SPECIAL SUPPLEMENT*

*To The Gazette of the United Republic of Tanzania No. 25 Vol. 104 Dated 17th October, 2023*
Printed by The Government Printer, Dodoma by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA. 752A la tarehe 17/10/2023

SHERIA YA TAFSIRI YA SHERIA,
(SURA YA 1)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 26(3))*

AMRI YA KUREKEBISHA MAKOSA YA KIUCHAPAJI KATIKA SHERIA YA UNUNUZI WA UMMA YA MWAKA 2023

Jina na kuanza kutumika Sheria Na. 10 ya mwaka 2023

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurekebisha Makosa ya Kiuchapaji Katika Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023 na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika tarehe 6 Oktoba, 2023.

Marekebisho ya makosa ya kiuchapaji

2. Makosa ya kiuchapaji yaliyomo katika kifungu cha 61 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, 2023 yanarekebishwa kama ifuatavyo:

(a) kwa kuongeza kifungu kidogo kifuatacho mara baada ya kifungu kidogo cha (2):

"(3) Endapo ushirika utakaoanzishwa kwa mujibu wa kifungu hiki utahusisha kampuni ya kigeni, kampuni ya ndani itakuwa ndiyo kampuni kiongozi na ushirika huo utapata

upendeleo kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii."; na

(b) kwa kubadili mpangilio wa kifungu kidogo cha (3) kuwa kifungu kidogo cha (4).

Dodoma
17 Oktoba, 2023

ONORIUS JOHN NJOLE
Mwandishi Mkuu wa Sheria